## MPANGO NA BAJETI YA HALMASHAURI YA WILAYA YA MPWAPWA KWA MWAKA 2019/20-2021/22 SEKTA YA KILIMO, UMWAGILIAJI NA USHIRIKA, MIFUGO NA USHIRIKA NA ARDHI

### 1.0 UTANGULIZI:

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Katika kuandaa Mpango na Bajeti ya mwaka 2019/20 Halmashauri ya Wilaya Mpwapwa imetumia miongozo mbalimbali katika kufanikisha kazi hii, Aidha utaratibu wa kuandaa mpango shirikishi wa Fursa na Vikwazo kwa Maendeleo (O & OD) ulizingatiwa katika kuibua miradi inayotokana na jamii katika ngazi ya Kata na Vijiji. Miradi ambayo itatekelezwa katika ngazi ya Kata na Vijiji imetokana na vipaumbele vya jamii kwa mfumo wa O & D.

Bajeti ya mwaka 2019/20 imezingatia mambo yafuatayo: -

**Miongozo mbalimbali**

1. Mwongozo wa uandaaji wa Bajeti uliotolewa na Wizara ya fedha na Uchumi mwezi oktoba 2018 na Amri/Agizo namba 15, 16, 17 na 19 cha kanuni za fedha za Serikali za Mitaa (The Local Authority financial memorandum) 2009,
2. Agizo namba 15,16,17 na 19 Kanuni ya fedha za Serikali za Mitaa 2009 (The Local Authority financial memorandum) vimezingatiwa katika kuandaa makisio haya
3. Agizo 16(2) ambalo linataka jumla ya makisio ya matumizi ya kawaida kulingana na Jumla ya makisio ya mapato (MATUMIZI = MAPATO) limezingatiwa.
4. Mwongozo wa kuandaa Mpango na Bajeti 2019/20.
5. Dira ya Maendeleo ya Taifa 2025.
6. Mpango wa Maendeleo wa miaka 5 (2016/17 – 2021/22)
7. Ilani ya Uchaguzi ya CCM (2015-2020)
8. Malengo endelevu ya maendeleo (SDG)

**Mahitaji muhimu**

- Uwekezaji wa Halmashauri ili kuongeza vyanzo vya mapato
- Kasi ya ongezeko la maambuki ya VVU kutokana na idadi ya watu.

### MAKADIRIO YA BAJETI KWA MWAKA 2019/20-2021/22

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Kwa mwaka wa fedha 2019/20 Halmashauri ya Mpwapwa inakadiria kutumia kiasi cha shilingi **191,909,180.00** kutekeleza shughuli zilizopangwa katika sekta za Kilimo Umwagiliaji na Ushirika, **shilingi 81,909,180.00** kwa ajili ya Sekta ya Mifugo na Uvuvi na shilingi **60,000,000.00** kwa ajili ya Ulipaji wa Fidia ya Ardhi. Aidha, Halmashauri imepanga kutumia fedha za ndani **shilingi 60,000,000.00** kwa ajili ya kupima viwanja vya Makazi, Biashara na Uwekezaji ili kuongeza mapato ya ndani ya Halmashauri pamoja na kukuza Uchumi wa Wilaya ya Mpwapwa kupitia Biashara na Uwekezaji.

**Mheshimiwa Mwenyekiti,**

Kwa msingi huo, naomba kuwasilishe Muhtasari wa bajeti ya sekta ya Kilimo Umwagiliaji na Ushirika, Mifugo na Uvuvi pamoja na Ardhi yenye jumla ya **shilingi 191,909,180.00** kwenye baraza lako ili iweze kujadiliwa na kupata maoni**.**

**Naomba kuwasilisha.**

Nackam H. Nchimbi
AFISA MIPANGO
**HALMASHAURI (W)**
**MPWAPWA**

**UENDELEZAJI WA BARAZA LA BIASHARA BAADA YA LIC KUMALIZA MUDA WAKE**

1. **UTANGULIZI**

   Mhe. Mwenyekiti tangu mwaka 2015 baraza limekuwa likiwezeshwa katika vikao na kazi zake mbalimbali na mradi wa kuboresha mazingira ya Biashara na uwekezaji (LIC). Kupitia LIC baraza limeweza kuhuishwa na kufanikisha miradi mbalimbali pamoja na kuboresha mazingira ya Biashara na uwekezaji. Shukurani za dhati ziwaendee LIC kwa juhudi zao za kuboresha mazingira ya Biashara na uwekezaji katika Wilaya ya Mpwapwa.

2. **MAPENDEKEZO YA UENDELEZAJI WA BARAZA LA BIASHARA BAADA YA LIC**

   Mhe. Mwenyekiti wakati LIC wakimaliza muda wake katika Wilaya yetu ni vyema sasa Halmashauri ikatafakari namna gani baraza la biashara linaweza kuendelea kufanya kazi kwa juhudi katika kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji hii ikiwa ni pamoja na kuendelea kufanya vikao vya majadiliano kati ya sekta ya umma na sekta binafsi, kuibua fursa mbalimbali za kibiashara na uwekezaji pamoja na kunadi fursa hizo ndani ya Wilaya na nje ya Wilaya.

3. **USHAURI**

   Mhe. Mwenyekiti kamati tendaji ya baraza la biashara kupitia kikao chake kilichofanyika tarehe 06/03/2019 inaiomba Halmashauri sasa ichukue nafasi ya LIC kuendeleza baraza la biashara kwa kutekeleza majukumu yaliyokuwa yakifanywa na LIC ambayo ni pamoja na;

   - Kugharamia vikao vinne vya baraza la biashara kila mwaka
   - Kugharamia vikao vinne vya kamati tendaji ya baraza la biashara kila mwaka
   - Kugharamia vikosi kazi mbalimbali vinavyoundwa katika vikao vya baraza la biashara
   - Kugharamia shughuli za ofisi ya baraza la biashara (shajala)
   - Kugharamia posho(mshahara) ya mratibu wa baraza la biashara kwa mwaka mzima

Mhe Mwenyekiti naomba kuwasilisha.

Consalva Sindato
Mratibu baraza la biashara (W)

**TAARIFA YA BARAZA LA BIASHARA**

**UTEKELEZAJI WA MAAZIMIO YA BARAZA LA BIASHARA KWA MWAKA 2018**

| TAREHE YA KIKAO | AGENDA /HOJA ZILIZOIBULIWA | MAKUBALIANO YALIYOFIKIWA | UTEKELEZAJI/MAFANIKIO | CHANGAMOTO |
|---|---|---|---|---|
| 08.01.2018 | Kupitia taarifa ya utekelezaji wa baraza la Biashara kwa mwaka 2016/2017 | Kutokana na baraza kuwa na wajumbe wengi wapya, ni vyema mafunzo kuhusu baraza la Biashara yakafanyika kwa wajumbe wote ili waweze kutekeleza wajibu wao ipasavyo. | • Tarehe 23/01/2018 mafunzo yalifanyika kwa wajumbe wa baraza la Biashara sekta binafsi. Mafunzo yaliwezeshwa na wataalamu kutoka LIC. Pia LIC iligharamikia gharama zote za mafunzo. Mafunzo hayo yalijikita katika ;<br>✓ Mafanikio ya baraza la Biashara kwa mwaka 2017<br>✓ Utekelezaji wa maazimio mbalimbali yatokanayao na vikao vya baraza la biashara<br>✓ Namna ya kuandaa ajenda<br>✓ Mashirikiano ya sekta binafsi katika kuandaa ajenda na kujenga hoja katika kikao cha baraza la biashara<br>• Tarehe 18-20/02/2018 mafunzo yalifanyika kwa wajumbe wanawake wa sekta binafsi mjini Dodoma. Mafunzo yalitolewa na chemba ya | Hakuna |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | wanawake wafanyabiashara Tanzania (T.W.C.C), mafunzo hayo yaligharamikiwa na LIC. Mafunzo yalihusu;<br>✓ Sera ya mwanamke Tanzania<br>✓ Namna ya kutunza fedha na kuweka kumbukumbu sahihi za biashara<br>✓ Fursa za Biashara kwa wanawake<br>✓ Mikopo kutoka mfuko wa Rais<br>✓ Urasimishaji biashara<br>✓ Kuongeza thamani katika Biashara<br>✓ Ushiriki wa wanawake katika baraza la biashara<br>• Tarehe 13/03/2018 mafunzo yalifanyika kwa wajumbe wa sekta binafsi baraza la Biashara. Mafunzo yalifanywa na wataalamu kutoka lic. Gharama za mafunzo ziligharamikiwa na LIC mafunzo yalihusu;<br>✓ Ushirikiano wa serikali ya Dernmark na serikali ya Tanzania kupitia mradi wa LIC<br>✓ Vikwazo katika Biashara na uwekezaji kupitia tafiti iliyofanywa | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | | na LIC 2014/2015/2016.<br>✓ Namna bora ya kujaza fomu za ufadhili wa mradi LIC<br>• Tarehe 14/03/2018 funzo yalifanyika kwa wajumbe sekta ya umma. Mafunzo yalihusu;<br>✓ Ushirikiano wa serikali ya Dernmark na serikali ya Tanzania kupitia mradi wa LIC<br>✓ Vikwazo katika Biashara na uwekezaji kupitia tafiti iliyofanywa na LIC 2014/2015/2016.<br>✓ Wajibu wa halmashauri katika kuandaa mazingira bora ya Biashara na uwekezaji<br>✓ Namna bora ya kujaza fomu za ufadhili wa mradi LIC | |
| | Kupitia changamoto na vikwazo katika Biashara na uwekezaji zilizowasilishwa na wajumbe sekta binafsi baraza la Biashara kutoka katika ziara yao ya mafunzo na kujitambulisha kwa wafanyabiashara | Kila mkuu wa idara achambue changamoto iliyowasilishwa kulingana na idara yake kisha kuwasilisha taarifa ya utatuzi au mpango mkakati wa kiutendaji katika kikao kijacho, | • Kuhusu ukosefu wa upatikanaji huduma ya TIN namba, ofisi ya TRA mkoa imefanya mazungumzo na makubaliano na LIC ili LIC iweze kununua mashine ya kutolea TIN na hatimaye kuzisambaza wilayani, kwa sasa mashine hiyo imefika | Hakuna |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | wenzao katika kata 16 wilayani Mpwapwa . changamoto hizo ni pamoja na;<br>• Kukosekana kwa huduma ya upatikanaji wa namba ya utambulisho wa mfanyabiashara katika Wilaya, hali inayosababisha mfanyabiashara kusafiri umbali mrefu kufika Dodoma mjini kupata TIN, changamoto hii ni kikwazo kikubwa katika urasimishaji Biashara.<br>• Ukosefu wa mzani wa kupimia wanyama katika minada<br>• Ukosefu wa elimu ya urasamishaji | | wilayani hivyo TIN zitapatikana hapahapa wilayani.<br>• Kuhusu mizani ya wanyama, kutokana na uharibifu mkubwa uliofanywa na wafugaji katika mizani iliyowekwa awali, wakulima wanashauriwa kutumia tepu kupima urefu wa ng,ombe ili kupata thamani halisi ya mnyama.<br>• Kuhusu taratibu za urasimishaji ardhi, wananchi wamepewa utaratibu unaopaswa kufuatwa ili kurasimisha maeneo yao aidha barua yenye kumbukumbu namba HW/MPW/L.40/35/77 imewasilishwa katika serikali za vijiji zikieleza utaratibu wa kurasimisha maeneo<br>• Kuhusu ukosefu wa soko la mazao katika Wilaya, Halmashauri imetenga ekari 20 katika kijiji cha Msagali kwa ajili ya kuanzisha soko la mazao.<br>• Kuhusu ucheleweshwaji wa pembejeo, halmashauri itahakikisha utoaji wa pembejeo | |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | ardhi.<br><br>• Ukosefu wa soko la mazao<br><br>• Uchelewesh waji wa pembejeo za kilimo | | mapema pale itakapopata gawio la pembejeo. Hata hivyo kwa mwaka 2018 serikali imetoa ruzuku katika mbolea mbili, mbolea aina ya UREA and DAP zitauzwa katika maduka ya pembejeo kwa bei ya<br><br>DAP- mfuko wa 50kg kwa Shs 51,344/= na UREA mfuko wa 50kg kwa Shs 38,890/= | |
| 09/02/2018 | Kusaini hati ya mashirikiano kati ya baraza la Biashara na baraza la madiwani | Hati ya mashirikiano ilisainiwa kwa makubaliano yafuatayo;<br>• Kikao cha pamoja kati ya baraza la Biashara na baraza la madiwani kiwe kinafanyika mara moja kwa mwaka mwezi wa tisa.<br><br>• Halmashauri itahakikisha baraza la Biashara linakuwa na chanzo cha mapato ili baraza liweze kuendelea baada ya LIC kumaliza muda wake.<br><br>• Maazimio yote ya kikao cha baraza la | • Ratiba ya vikao vya baraza la Biashara kwa mwaka 2018 imeandaliwa na kikao cha baraza la madiwanai na baraza la Biashara kitafanyika mwezi wa tisa .<br><br>• Kuhusu baraza la biashara kuwa na chazo cha mapato ili kuendesha shughuli la baraza la pindi LIC watakapoondoka, bado halijafanyiwa kazi. | Hakuna |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | Biashara yatakayohitaji maamuzi/ushauri wa baraza la madiwani yatawasilishwa katika kikao cha baraza la madiwani . pia maendeleo ya baraza la Biashara yawe yanawasilishwa katika vikao vya baraza la madiwani.<br><br>• Wenyeviti watano wa kamati za kudumu katika baraza la madiwani wawe wajumbe wa kudumu katika baraza la Biashara. | • Agizo limezingatiwa<br><br>• Agizo limezingatiwa, sasa wenyeviti wa kamati za kudumu wanahudhuria vikao vya baraza la Biashara | |
| | Hali ya miradi inayofadhiliwa na LIC | LIC watoe mafunzo namna ya uandishi wa miradi kwa wajumbe wa baraza la Biashara wote ili kuongeza ufahamu wa uandishi mzuri wa miradi na kuwezesha halmashauri kuwa na miradi mingi na kuongeza kipato kwa wanachi kupitia mazingira bora ya Biashara na uwekezaji. | LIC ilitoa mafunzo ya uandishi miradi kwa kutumia fomu maalumu(SIFF concept note) tarehe 13-14/03/2018 kwa wajumbe wote wa baraza la Biashara. | Hakuna |
| 30/04/2018 | Umeme usiotosheleza katika eneo la viwanda mjimpya | Ofisi ya Tanesco Mpwapwa itoe mpango kazi wake wa kuboresha umeme eneo la viwanda mjimpya kwa kufunga transfoma kubwa ya umeme wa viwanda. | Transfoma kubwa ya umeme wa viwanda imefungwa eneo la viwanda mjimpya mwezi Julai, 2018. | Hakuna |
| | Taarifa ya maendeleo ya kituo cha kilimo kibakwe. | Vyuo vya kilimo (Visele na LITA) watengeneza mashirikiano na chuo cha WARC kibakwe, katika kuboresha vyuo na kupeana uzoefu kwa kueleza nini kila chuo kinafanya katika kikao | Vyuo vya kilimo vitaalikwa katika kikao cha baraza la Biashara na kunadi fursa na huduma zinazotolewa katika vyuo hivyo. | Hakuna |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | kijacho. | | |
| | Ushiriki wa SIDO katika kukuza Biashara na uwekezaji Wilaya ya Mpwapwa . | Kiundwe kikosi kazi kitakachoshirikiana na SIDO katika kuibua na kukuza kongano wilayani.<br><br>Kikosi kazi kilipewa majukumu yafuatayo;<br>• Kuandaa hati ya mashirikiano na SIDO mkoa kuhusu kukuza viwanda vidogovidogo na kongano wilayani Mpwapwa<br>• Kujifunza zaidikuhusu kongano na kufanya utekelezaji huo katika Wilaya kwa kuhamasisha uanzishwaji kongano.<br>• Kupata mtaalamu kutoka SIDO atakaye ratibu shughuli za SIDO Wilaya. | Kikosi kazi cha wajumbe 6 ikiwa watatu toka sekta binafsi na watatu toka sekta ya umma kiliundwa. Aidha baada ya SIDO kufanya maandalizi ya mafunzo waliomba Wilaya itoe watu watatu tuu kati ya wajumbe wa kikosi kazi, kikosi kazi kilipata mafunzo ya kongano Mbeya tarehe 03-08/09/2018. Kwasasa kikosi kazi kimeandaa mpango kazi wa namna ya kuanzisha kongano wilayani na utekelezaji unatarajiwa kuanzi katikati ya mwezi Desemba baada ya kuwezeshwa na LIC. | Hakuna |
| 09/11/2018 | taarifa ya ujenzi wa miundombinu ya mnada wa mifugo katika kijiji cha ilolo | Kuwepo na muhtasari wa kikao kilichofanyika juu ya kuwepo kwa mradi huo<br><br>Uwasilishwe mkataba ambao utaonesha kuwa umesainiwa tarehe ngapi na mwezi gani na mradi unategemewa uwe umamalizika lini. | • Agizo limezingatiwa, mkataba na muhtasari vitawasilishwa katika kikao kijacho | Hakuna |
| | taarifa ya maendeleo ya kituo cha warc-kibwakwe | Uongozi wa halmashauri uweke mikakati stahiki ya uendelezaji wa kituo ili kiweze kuwa na manufaa zaidi katika Wilaya na kufahamika kwa jamii | Agizo limezingatiwa, halmashauri imeaandaa muongozo kwa ajili ya kutoa mafunzo kwa wakulima wa mazao mbalimbali pia kwa kushirikiana na wengine | Hakuna |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| | | nzima. Kufanya hivyo itasaidia hata kuwa na mashirikiano na vyuo vingine vya kilimo na mifugo. | ikiwemo wizara ya kilimo, SUGECO, wameonyesha nia ya kutumia kituo cha kibakwe kwa ajili ya kuwajengea uwezo vijana katika kilimo. Ili kuwa na muendelezo mzuri idara ya kilimo imependekeza jina la mtumishi atakaesimamia kituo ili kujiendesha kama chuo | |
| | taarifa ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji skimu ya lumuma (kitati na mafene) | Wajumbe walipokea taarifa iliyowasilishwa na kuipitisha | | Hakuna |

**MPANGO KAZI WA BARAZA LA BIASHARA KWA MWAKA 2019**

## 1. UTANGULIZI

Mhe. Mwenyekiti baada ya kusikiliza na kuona taarifa ya baraza la biashara kwa mwaka 2018 ikiwa imeeleza agenda zilizoibuliwa, maazimio na utekelezaji wake, ni vyema sasa baraza hili la biashara likaweka mapendekezo yake ya mpango kazi wa baraza la biashara kwa mwaka 2019 ili kuwa na muongozo mzuri utakaofanyiwa kazi mwaka mzima .

Mhe. Mwenyekiti kamati tendaji ya baraza la biashara, katika kikao chake cha tarehe 06/03/2019 kilipendekeza mambo yafuatayo yafanyiwe kazi kwa mwaka 2019 na kukamilika;

| NA | KAZI | MUHUSIKA | MUDA WA KUKAMILISHA |
|---|---|---|---|
| 1 | Kukamilisha rasimu ya mpango wa kitovu cha biashara (commercial hub) | Halmashauri | Juni 2019 |
| 2 | Kukamilisha rasimu ya upimaji wa eneo la viwanda (visele) | Halmashauri | Julai 2019 |
| 3 | Baraza la biashara kwa kushirikiana na Halmashauri litasimamia uanzishwaji wa ushirika katika maeneo ya mabonde yanayolima mazao ya kitunguu na pia katika maeneo yanayolima korosho | Halmashauri | Desemba 2019 |
| 4 | Kukamilisha taratibu za kisheria za upatikanaji wa eneo la soko la mazao kiwilaya | Halmashauri | Julai 2019 |
| 5 | Kurasimisha ardhi katika maeneo ya vijijini | Halmashauri | Desemba 2019 |
| 6 | Kukamilisha ujenzi wa miundombinu ya mifereji ya umwagiliaji | Halmashauri | Desemba 2019 |
| 7 | Kuendelea kufanya vikao vya kawaida vya baraza la biashara na kiako cha baraza la biashara na madiwani kwa kufuata ratiba ya baraza la halmashauri siku moja baada ya baraza la waheshimiwa madiwani | Halmashauri | Endelevu |